# BUNDI MDOGO

**Lene Mayer-Skumanz / Austria**
**Salvatore Sciascia /Italy**
**Mtafsiri: Dr. David Maillu**



**Zamani za kale, wakati watu na wanyama walikuwa wanatumia lugha moja, kulikuwa na bundi mmoja wa kike na mdogo aliyeishi msituni ng'ambo ya milima ya ndoto. Alikuwa mmoja wao dada na ndungu zake sita. Ndiye alikuwa wa mwisho kuhama tunduni la mti moja mzee sana. Tunduni humo ndiko walikozaliwa. Wazazi wake walikuwa wamemfundisha kuruka kwa bidii. Wakamfundisha kuwinda panya na kuogelea katika mwangaza wa jua. Wakimfundisha, walizidisha kumwambia, "Bundi wetu mdogo, lazima huwe mhodari; maisha ni magumu na lazima ujitayarisha kupambana nayo." Naye akajitetea, "Mimi sio mdogo na muoga namna hiyo." Bundi wazazi wakaguzana midomo, halafu wakamjibu, "Basi, wajua nini? Bundi Mwenyezi muumbaji wa kila kitu atakulinda mahali kote utakakoenda. Tumekufundisha amri zote. Moja wa amri hizo ni kwamba, katika uwindaji wako, jaribu kuua upesi iwezekanavyo ili mwenye kuuawa asiwe na maumivu yoyote, na nyama yake iwe tamu. Na ili huwe unaweza kuruka kwa safari ndefu, endelea kufanya mazoezi makubwa makubwa. Kwa hayo yote, sisi wazazi wako, twambia hatuna mengine. Bundi Mdogo alipindua uso wake nyuma na kuwaangalia wazazi wake kwa mara ya mwisho. Ndipo akarusha sauti ya kuwaaga kwaheri, akajitupa, akapanua mabawa yake na kuruka.**

**Huko ng'ambo ya msituni wa ndoto kulikuwa kichaka kikubwa. kuliishi wanyama wengi sana wa kila aina. Baada ya kuruka kwa muda, Bundi Mdogo aliona mahari pazuri pa kutua. Palikuwa juu ya jiwe moja pana. Akateremka vizuri na kutua penye majani kidogo kidogo. Akaaga jua kwaheri sababu ilikuwa inatua. Mwenyewe alikuwa na furaha ya kuwa huru. Kwenye jiwe hilo, hapo chini akamwona Paka wa msituni naye akiota jua la jioni na kujifurahisha pia. Huyo Paka alikuwa na alama nyeusi za mstari zilizoanzia puani na kwenda juu kichwani. Wakati huo mkia wake**

wenye manyoa mengi, ukiwa umejipinda, ulitetema kidogo akimwangalia Bundi Mdogo. Akasema, “Bundi, umefika wakati mzuri. Hebu niambie, yawezekanaje Paka Mwenyezi muumba yote, awe anawezake kukubali paka wengine ati wawe wanafugwa na watu?” Naye Bundi akaimba wimbo majibu ya kumshtua paka akisema, “Namna gani? Jana niliruka safari yangu ndefu sana maishani mwangu. Mwishowe nikateremka nikipigana na upepo mkali kutoka milimani ya ndoto. Njiani nikaona nyumba ya mawe na miti yenye kujengwa na wanadamu. Nyumba ilizungukwa na kuku tamu wa kike na jogoo. Lakini, sababu nilikuwa nimekula nikashiba, niliwaangalia tu nikiwa hewani. Wakati huo huo, niliona mwanadamu akiwa ameketi nje ya nyumba ati akimguzaguza paka aliyekuwa ameketi pajani mwake. Paka hakumuuma ama akatumia kucha zake kumuumiza binadamu, lakini alitulia na kuitikia kwa sauti ya mapenzi. Nilistaajabu kabisa kuona, ati paka kama wewe, huwe umejipeana kwa binadamu awe anakushika shika ukimwimbia sauti ya mapenzi, kkrrrrr!



Hayo yanawezekanaje?” Kusema hivyo Bundi akaruka na kutua kwa kwa mti, tena akapindua uso wake na kumwangalia paka wa mwituni. Paka alikuwa amemjibu, “Naweza kujua hayo namna gani mimi?” na baada ya kumjibu akainuka, mkia wake ukijipinda kwa kufura, macho yake ya rangi kibichi yakapinduka pinduka yakionyesha rangi ya kimajano. Akamwuliza Bundi, “Lakini sababu gani ukaniuliza hayo Bundi? Akina Bundi ni watu werevu na wanajua majibu ya maswali yote duniani. Ya nini kuniuliza?” Akiwa na woga Bundi akamjibu, “Kusema kweli, hayo sijayajua.” Paka akamwuliza, “Hujui hayo na hali unaishi? Aibu kubwa sana kwako, ruka basi ukapotelee mbali.” Bundi mdongo hakuwa na mengine ya kusema. Alijitupa hewani na kuruka mpaka alipoona mti mwingine mkubwa wenye tundu limepanuka vizuri. Palikuwa mahali pa kufutia zaidi jioni hiyo. Akateremka na kutua hapo hapo, halafu akaangalia kuzunguka. Akasikia sauti ya mabawa yakipigana na, mara moja, tausi mmoja akatua hapo hapo karibu. Uzito wake ukatingiza matawi ya mti.



**Tausi alitua akijiambia, “Ah, mwishoni nimefika! Nimechoka sana, lazima nipumzike na kulala. Lakini, sababu gani niwe siwezi kuruka kwa umaridadi kama ninavyotembea?” Mara akaona mgeni na kuuliza, “Hala, nani huyu mwenye kuketi hapa? Hei, kitoto hiki, sikiliza. Hapo unapoketi ndipo kwangu ninapolala.” Bundi akamjibu, “Nasikitika, hayo sikuyajua.” Tausi akapanua mkia wake juu na kuutingiza akisema, “Kumbe ni Bundi, nakusikia kwa sauti yako nzuri zaidi. Sio vibaya,” akakunja mkia wake vizuri na kuuacha ukiniginia. Akamwambia Bundi, “Nina swali moja ambalo lazima nikuulize. Je, kwa nini Tausi Mwenyezi muumbaye wa yote, hakupeana miti ya kutosha kwa kila mmoja wetu hawe na mahali pake?” Naye Bundi akamjibu, “Ati wasema nini?” Tausi akasema, “Wajua nini? Ijapokuwa nina mkia maridadi ninaoweza kuupanua vizuri uonekane na kupendeza kila jicho, inapotaka kulala, huo mkia unaniletea taabu nyingi sana. Lazima niutafutie mahali pazuri juu ya miti mikubwa ndipo naweza kulala vizuri mkia wangu ukiwa melalishwa. Kunayo miti michache sana ya kunipa nafasi ya kunitosha.” Bundi akamjibu, “Basi naona unayo nafasi nzuri sana juu ya mti huyu.”**

**Naye Tausi akasema, “Ndio, lakini ningetaka kuwa na miti mitatu au mine ili niwe naweza kuchagua, sababu gani hayo hayakuwezekana?” Bundi akasema, “Waniuliza mimi? Sijui.” Kusikia hivyo Tausi akafikiria, akajipinda kidongo na manyoya yake ya samawati ya ufalme wake yakamguza Bundi kifuani. Halafu akamwuliza, “Hati hujui? Sababu gani hujui na hali Bundi wanajua majibu ya maswali yote duniani?” Naye Bundi akamjibu, “Kusema kweli, sikujua hayo ni mambo ya ulimwengu.” Ndipo Tausi akamtukana, “Mjinga Bundi Mdongo wewe! Wewe sio Bundi kamili! Aibu kubwa kwako. Basi ruka na uende ukateketee.” Bundi aliposikia hayo, alishtuka sana. Kwa hivyo akaruka na kwenda kabisa. Mwishowe akakuta shimo ndogo katikati ya mawe. Akatua na kuingia hapo ndio apumzike na kufikiria juu ya maisha yake. Akiwa hapo akajiuliza, “Je, sababu gani nione aibu? Na sababu gani ati niwe nayajua majibu ya maswali yote ulimwenguni? Kwanza, sababu gani Paka akasema Paka wa Mwituni Mwenyezi muumba yote? Tena naye Tausi akasema juu ya Tausi Mwenyezi muumbaji wa yote ya ulimwengu? Kwani wao hawajui ni Bundi Mwenyezi peke yake muumbaji wa yote ulimwenguni?” Wakati huo jua lilikuwa limetua huko ng’ambo ya milima ya ndoto. Na huko mashariki nyota moja ya kung’ara kabiza ikawa imejitokeza**

**na kupanda kufikia juu ya miti. Mwangaza wa nyota ukawa umemfikia kupitia ghuba ndogo, na kumfanya Bundi kujiona akiwa na rangi ya fedha.**



**Akajiambia, “Naam, sasa ndio wakati wangu wa kwenda kuwinda, kwani ni usiku kamili. Namshukuru naye Popo Mwenyezi muumbaji yote ulimwenguni.” Akisha kusema hivyo akainua macho na kumwona Popo mmoja mwenye kuning’inia akijishikila kwa jiwe. Kwa hivyo, ili apate mabawa ndio aruke vizuri, akayapanua na kuchezacheza nayo. Lakini wakati huo huo kukatokea maji mazito katika mwanya. Yakamwangukia kwa pua na kutambaa mwilini mwake. Akalia, “Fiu! Yananukia vibaya!” Popo naye akamjibu, “Ndio, yananukia vibaya sana. Kwa sababu hiyo, mwili wangu hauna nyama nzuri kuwa chakula chako. Wewe si Bundi tu?” Bundi akamjibu, “Naam, lakini Bundi Mdogo.  Kwa hivyo huenda nikawa sio Bundi kamili.” Popo akalia, “ Bah, bah, bah! Bundi ni bundi. Bundi wana majibu ya maswali yote duniani.” Akapindua sauti yake na kusema, “Lakini, nina swali moja ningeteka kukuuliza. Niangalie vile nimeumbwa kwa umaridadi sana, nikawa nimepewa vitu vyote. Maana yake naweza kujitafutia midudu hata kwa giza kubwa namna gani.**

**Natamka maneno tu, na sauti yangu inaanza mwendo mpaka itakapomkuta mdudu, ndipo inanirudia kuniambia mdudu ako upande gani. Halafu namrukia na kumkamata na kumla. Lakini, kuna jambo moja linalonitia hofu sana. Wajua nini? Bundi akamjibu, “Niambie.” Naye Popo akamjibu, “Najipatia mtoto mmoja tu kwa mwaka mzima na hali vipepeo vinataga mayai mengi sana. Hata hawa nungunungu wanazaana sana. Na hata mbwa mwitu anaweza kujipatia watoto watatu. Je, sababu gani Mwenyezi Popo muumbaji wa kila kitu duniani ati awe anapata mtoto mmoja tu?” Bundi akamjibu, “Sijui kamwe.” Kusikia hayo Popo akashtuka na mwili ukayumbayumba. Akamwuliza, “Jamani, ati hujui? Wataka niyaamini unayosema?” Bundi akasema, “Nakwambia ukweli, sijui.” Na hata akakasirika akijiuliza sababu gani hata Popo hawezi kumwamini. Popo akamfuata kwa kumwuliza, “Kama kweli hujui, nani anaweza kujua? Labda sababu hutaki kufikiria vizuri. Sivyo? Labda utanirudia na jibu wakati utakuwa na fikira changamfu.” Bundi akamjibu, “Ukitaka hivyo, basi tuyaache hapo hapo.” Baada ya kusikia hayo Popo akaruka akiitoa hile hile sauti yake ya kuwinda wadudu. Akapotea gizani kulikokuweko na Popo wengine.**



**Bundi akawaangalia vile waliruka, wakikata njia na kupitana kila mahali katika bala mwezi. Mwishowe Bundi akaona, hata akiwa anaudhika namna gani, lazima ajitafutie chakula. Maana yake njaa ilimzidi. Kwa hivyo naye akaruka akaende kuwinda. Haikuwa rahisi kwake, lakini alitumia akili yake yote. Akamrukia panya mmoja kama radi, akamuua na kumla. Aliposhiba na akaona hata chakula kimebaki. Akiwa hapo alisikia sauti ya panya wengine wakitembea humo shimoni. Akauliza, "Panya, niambieni, je, nguvu za nani zilizomuumba nyinyi" Ni nguvu za nani zilizoumba kila kitu?" Jibu la swali lake likatoka huko chini, "Nguvu zake Mwenyezi Panya, hakuna nguvu za mwingine. Hata hayo unayajua wewe Bundi, mwenye kujua mambo yote duniani. Kwani unaniuliza kwa upembelezi ndio nitoke shimoni unishike na unile? Ukoo wenu twaujua sasa sana. Mmoja wetu akipotea, twajua ni nani wa kulaaniwa. Ni Bundi. Labda ungeniambia ni kwa sababu gani nyinyi Bundi hamkuumbwa watu wa kula nyasi?" Bundi akamjibu,**
**" Hama tukaumbwa watu wa kula nafaka, sivyo?"**




**Panya akainua sauti akisema, “La, nafaka ni yetu.” Baada ya maneno hayo, Bumdi akaruka na kutua juu ya mti kupumzika akiimba, “Tuwit, tuwuu, mimi sio mjuaji wa mambo yote. Mimi ni mtu hajui chochote, hayo nayajua kweli.” Lakini huko chini akaona kivuli cha mtu mwenye mkia umekunjwa akipita. Mwenye kupita akasema, “Kumbe, lakini ngojea, kwani mpaka sasa umepata ujuzi angalau kidogo kama uzi wa ndevu.” Bundi akamfuata mwenye kusema na kumjibu, “Naam, nitasoma na kuyajua mengi.” Wakati huo usingizi ulikuwa umemwingilia. Akalala fofo mpaka asubuhi mapambazuko, wakati aliona mwangaza unamjia katikati ya matawi. Akafurahia hayo mapambazuko na kujiuliza, “Je, leo nitapata ujuzi wa namna gani?” Ndipo akajitupa na kupanua mabawa yake, akaruka kwa mwendo kimya akipita kukiwa na baridi ya asubuhi, mpaka akafika milimani ya ndoto. Akiwa huko juu, akaona mto wenye kupitisha maji yenye povu la kumetemeta. Akateremka na akaiona hile nyumba paka mwitu aliyozungumzia. Kila kitu mahari kulikuwa kimya, mbali ni kuku wachache walikuwa wanakibizana na nyungunyungu wapate chakula. Na kwa umbali kidogo wimbo ulisikika. Bundi akafuata sauti hio ya kufurahia kwa utaratibu. Mwishowe akakuta mwanamke akichota maji na kuiweka kwa ndoo. Bundi akakaa chini mahali kuna kijiti chenye matawi. Akauliza kwa upole, “Kwani una sauti nzuri kuliko yangu?”**



**Mwanamke akasimama, akacheka na kusema, “Hebu jaribu kufikiria, kama kweli viumbe vyote duniani vingekuwa na tabia moja, hiyo ingeweza kuaribu umaridadi wa maisha. Kwa mfano, wewe umefanikiwa ukawa unaweza kuona na kusikia vizuri kunishinda, na hata ukapewa kipawa cha kuruka.” Bundi akauliza, “Je, kwa nini unaimba?” Mwanamke akamjibu, “Naimba nikifurahia ama nikisherekea kazi yangu. Pia kuna wakati mwingine naimba nikimpa Mama-mkuu heshima kwa kuumba kila kitu.” Bundi akauliza, “Huyo Mama-mkuu anaishi wapi?” Mwanamke akamjibu, “Anaishi kila mahali. Macho ya mwanadamu haiwezi kumuona. Jua, mwezi na nyota ni nguo zake za dhahabu.” Bundi akasema kwa upole, “Je utasema nini nikikuambia kwamba hata samaki wanajua Samaki-mkuu aliyeumba kila kitu duniani? Mwanamke akamjibu, “Mama-mkuu hawezi kukasirika sababu anakipenda kiumbe chote duniani.” Bundi akapindua kichwa na kumwuliza, “Je unavyoimba, huyo Mama-mkuu anafurahia wimbo wako?” Mwanamke akamjibu, “Ni matumaini yangu kwamba wimbo wangu unampendeza. Pia, mimi nimemuomba vitu nyingi. Moja wazo ni kwamba paa la nyumba langu lidumu kwa**

**miaka mingi, na kuku wangu wa kike wazae kuku wengi, na tena mimi na watoto wangu tuwe na maisha mazuri." Bundi akauliza, "Je kinachotendeka kesho kinakusumbua?" Mwanamke Akajibu, "Naona kweli lazima tuwe tunasumbuka. Hakuna ajuaye kesho kutakuwa na taabu ama uzuri gani. Kwa mfano, sasa nataka nipate nguo zaku zimekauka, lakini sijui kama kutanyesha ama hakutanyesha karibuni?" Bundi akasema, "Kwa maoni yangu, hakutanyesha." Baada ya kusema hayo akajikwaruza na kuaga kwaheri. Akiaruka akielekea juu. Jua iliwaka siku yote. Bundi akafurahia kuoga jua siku yote akiwa anasingizia mambo yote vizuri sana. Jioni akaruka akielekea mteremko wa milimani ya ndoto. Jua lilipokuwa linatua, akaona kitu kinameta meta katika miti kama nyota ya dhahabu. Akakifuata kimulimuli hicho na kuona kilikuwa nyumba ya mbao. Mwangaza uliotoka katikati ya mbao za ukuta uliwavutia vipopo. Mwangaza ulimvutia Bundi sana. Akajaribu kukaribia mpaka akakaribia mwanzo wa ukuta. Akiwa hapo alifurahia joto kadiri mpaka akaamua kuimba wimbo wa upendo wa Bundi. Akarukaruka, akajimimina, akajikwaruzaruza akiufurahi wimbo wake. Sauti nzito kutoka kwa nyumba ikasema, "Bundi maskini, nakukaribisha kwa moyo mkunjufu." Bundi akashtuka.**

**Akaangalia sauti hiyo ilitoka wapi kando ya mwangaza. Kumbe ilitoka kwa mzee mwanamume. Bundi akamwuliza, "Hunafanya nini?" Mzee akajibu, "Nasoma." Akawafukuza vipopo kutoka kwa karatasi na kusema, "Siku ilikuwa fupi sana kwangu. Ndio sababu najaribu kusoma nikitumia mwangaza wa taa ya mkono. Hiki ni kitabu kinachousika na Baba-mkuu Mwenyezi, aliyeumba kila kitu." Bundi akauliza, "Je, huyo Baba-mkuu anaishi wapi?" Mzee akajibu, "Anaishi mahali pote mbinguni ambapo macho yangu hayawezi kuona. Anaishi ndani ya roho za watu." Bundi akauliza, "Unaweza kumwuliza kesho kutakuwaje?" Mzee akajibu, "Naam, unaweza. Na hata pia naweza kuongea naye juu ya mambo ya kale. Kuna mambo mengi maishani mwangu ambayo nayafanya lakini Baba-mkuu hawezi kukubaliana nayo.**
**Bundi akasema, "Je, nikikwambia kwamba Vipopo walijua Kipopo-kikuu Mwenyezi muumbaji wa kila kitu, utasemaje?"**



**Baba mzee akacheka na kujibu, "Wao wanawezaje kufikiri juu ya Baba-mkuu ninayesema juu yake kuwa mtu mwingine?" Bundi akajibu, "Huenda ikawa kama vile mama aliyekuwa akichota maji mtoni alivyomuelewa Mama-mkuu." Baba mzee**

akasema, “Nishamwambia mama huyo mambo mengi kuhusu Baba-mkuu lakini yote hakuyatilia maanani. Lakini hata hivo nina matumaini siku moja atajui ukweli wa maneno hayo.” Bundi akauliza, “Je, Baba-mkuu anakasirika mama huyo anapomuita Mama-mkuu?” Mzee akafikiria kwa muda mrefu. Mwishowe akamjibu, “Sifikirii hivo Baba-mkuu ni mkarimu, niko na hofu inaniumiza kidogo, lakini ni mtumishi mkarimu….” Bundi akamwambia, “Usijaribu kuyaacha yale yote unayo, kisha akaenda zake.” Siku iliyofuata Bundi alirudi kwa mto. Wakati huu hakumwona yule mwanamke lakini alimwona mtoto aliyekaa kando ya mto. Paka alimkalia mtoto pajani na miguu ya paka ikaning’ina na kugusa maji, paka akimwangalia samaki. Jua nalo lilimmlika mtoto, paka, mawe na nyasi vizuri sana. Bundi akatua juu ya mti bila sauti. Macho yake makali yaliona kila kitu wa umbali. Yakaona vile mtoto alivyompapasa paka na vile vile paka alivyofurahia kupapaswa mpaka akasahau mambo ya masamaki. Na akaona urembo wa mawimbi ya maji. Hayo yote yakamridhisha kweli kweli. Na hata akajiuliza, “Je, mtoto huyu ana jina la muumbaji aliyeumba kila kitu na hata akafanya jua liwake?”



Labda mtoto hakuwa na jina la FUMBO hilo, ijapokuwa mwenyewe aliishi ndani la FUMBO. Bundi alilisikia FUMBO hilo kabisa. Kesho na kesho kutwa hasikuwa na uhusiano naye na, kwa hivyo, hasikuwa na maana kamwe. Bundi Mdogo akapindua kichwa upande kwa mafikira makubwa na kuyakumbuka majina ya viumbe wa ajabu akisema: Wewe BUNDI-MKUU-AMBAYE-ALIUMBA-KILA KITU

MKUU PAKA MWITU

TAUSI MKUU

POPO MKUU

PANYA MKUU

MAMA MKUU

WEWE BABA MKUU, hata wewe unaweza kuitwa:

WEWE-SIRI-KUU-YA-NDANI-NA-MILELE.

Bundi akasema kwa sauti kubwa, “Sasa?” Paka aliposikia hivyo akafungua macho na kumwangalia Bundi. Akamkonyezea jicho na kummwimbia kwa unyonge, “Si ndio!”



**Baada ya jua kutua Bundi akaruka na kurudi msituni. Akalitafuta lile shimo la panya, akaiona na kuingia ndani akiimba imba, "Tu-wiiit, yu-wooo. Kila maisha yanaishi kwa maisha. Hata nafaka yako ni hai!" Bundi akiendelea kuruka akakutana na popo na kumwuliza, "Unaruka vizuri sana. Kama ungeruka ukimbeba mtoto mmoja ungekuwa mzito sana kuruka?" Naye popo akamjibu, "Huenda ikawa unayosema niya kweli." Bundi akaruka kupitia juu ya mti ule Tausi alipokuwa akilala na kufikiri, "Mwana shida huyo naye, mwenye ukoo wa mteteo wa kuku. Mwenyewe ni kama kuku tu, laknini ati hatosheki na miti moja wa kulalia." Akaendelea na kuruka na kumuona paka mwitu akilala katika sehemu kubwa la tawi katika uwindaji wake.**
**Macho ya paka yakamwakangalia na kumwuliza, "Je, sasa umekuwa mwelevu?"**



**Bundi akamjibu kwa furaha, "Sio sana bado ningali mtoto na naendelea kusoma. Hata hivo, leo nimuona paka amechiacha apapaswe. Hata samaki aliyekuwa hapo karibu mtoni hakumvutia atoke pajani la mtoto. Paka mwitu akalia, "Jamani, jambo mbaya sana hilo!" Akaongeza kuuliza, "Lakini kama kweli kila kiumbe kingejihisi**

**kama kile kile kingine tu, si maisha yangekuwa na uchovu mwingi? Sio ni sawa kwamba SIRI-KUU inayokufanya umuite PAKA-MWITU-MKUU inakubali watu waishi kwa njia nyingi?" Paka mwitu hakumjibu. Bundi akaendelea kuruka. Mwishowe akawaamkia wazazi wake nyumbani mtini. Wazazi wakamkaribisha kwa kumwuliza, "Je BUNDI-MKUU-AMBAYE-ALIUMBA-KILA KITU amekufanya usome mambo mengi?" Bundi Mdongo akawajibu kwa utulivu, "Ndio kweli alinifanya nisome mengi. Kutoka sasa nitakuwa nikimwambia nyinyi na kila kiumbe mambo mengi kuhusu jambo hilo." Mama Bundi akalia, "Mwambie kila mtu mwana waku." Baba naye akasema, "Lakini kwa binadamu itakuwa shida kwako kuwajulisha hayo. Kwa sababu hawamskilizi na kumwamini yeyote mmoja wetu." Bundi Mdogo akainanamisha kichwa chake upande na kulia kwa nguvu, "Nitaruka na kumtafuta, kama iwezekanavyo, mpaka siku moja nitapata binadamu wa kunisikiliza na kuniamini."**

